

Tume ya Utumishi wa Umma ilifanya mkutano wa uzinduzi wa Kamati ya UKIMWI ya Tume uliofanyika kuanzia tarehe 13/ 1/ - 17/02/2006 huko Arusha katika Chuo cha Afya (Centre for Education Development in Health in Arusha – CEDHA).

Lengo la Mkutano huo lilikuwa ni kuzindua kamati ya UKIMWI ya Tume, pamoja na Kamati ya UKIMWI kukabidhiwa majukumu yake rasmi. Pamoja na lengo hilo, wajumbe wa Kamati walipatiwa mafunzo ya siku tano ya jinsi ya kupambana na UKIMWI mahali pa kazi na kutakiwa kuwa chachu na kichocheo cha kubadili tabia (Behavior) katika suala zima la ngono holela.

Mafunzo hayo yalitolewa na wataalam toka sehemu mbalimbali kwa lengo la kupata uzoefu toka maeneo yao ya kazi ya namna wanavyopambana na ugonjwa huu hatari.

KWANINI KUNA UMUHIMU WA KUANGALIA MASUALA YA UKIMWI.

Nguvu kazi imekuwa inaathirika, hasara kwa Taifa. Ofisini kuna mchanganyiko wa wanaume na wanawake. Watumishi wanaishi katika Jamii. Hivyo ni muhimu kuchukua hatua ili kuona kuwa:

- Watumishi hawaathiriki
- Wanaoathirika hawakati tamaa ya maisha.
- Wanaoathirika hawafi mapema

MAJUKUMU YA KAMATI YA UKIMWI YA TUME YA UKIMWI.

Malengo ya Kamati ya Tume.

1. Kupunguza Uenezi wa VVU kwa watumishi wa Tume na familia zao.
2. Kushawishi viongozi wa Tume kutoa kipaumbele kwa masuala ya VVU/UKIMWI.
3. Kuondoa unyanyapaa na ubaguzi wa wenye kuishi na VVU/UKIMWI na kuhakikisha haki za binadamu za wenye VVU/UKIMWI zinazingatiwa.
4. Kero za VVU/UKIMWI kuunganishwa na kupewa kipaumbele katika mkakati wa Tume wa kupunguza Umaskini.
5. Kuongeza maarifa ya kujikinga na uambukizaji wa VVU kwa watumishi.
6. Kuhakikisha kuwa wanaoishi na VVU/UKIMWI wanapata matunzo na misaada.